

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Simu Nambari: 2152532/3  
Baruapepe: [cg@dcea.go.tz](mailto:cg@dcea.go.tz)  
Tovuti: [www.dcea.go.tz](http://www.dcea.go.tz)  
Nukushi: 2152820



8Barabara ya kivukoni,  
S.L.P. 80327,  
Dar es Salaam.

### TAARIFA KWA UMMA

**Dar es Salaam, 03 Juni, 2022:**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imekamata jumla ya kilogramu 877.217 za dawa za kulevya na kuzuia uingizaji wa kilogramu 122,047.085 na Lita 85 za kemikali bashirifu Nchini. Dawa za hizo ni heroin kilogramu 174.112 zilizowahusisha watuhumiwa wawili na bangi kilogramu 703.105 zilizowahusisha watuhumiwa sita ambao wote wamefikishwa mahakamani.

Aidha, tarehe 12 Mei 2022, katika eneo la Tabata relini wilaya ya Ilala, mkoa wa Dar es Salaam Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ilikamata Kilogram 174.77 za dawa ya kulevya aina ya heroin. Katika tukio hilo Salum Shabani Mpangula (54), kabila mngindo, dini muislamu, mkazi wa mtaa wa reli - Tabata ambaye ni Nesi msaidizi Karikoo Dispensary amekamatwa kwa tuhuma za kusafirisha dawa hizo.

Kufuatia upekuzi uliofanyika nyumbani kwa mtuhumiwa, paketi 162 zenye unga uliodhaniwa kuwa dawa za kulevya zilikutwa ndani ya viroba sita vilivyokuwa vimehifadhiwa chumbani kwa mtuhumiwa, na paketi moja ya unga huo ilikuwa imewekwa kwenye mfuko mweusi wa nailoni na kufichwa chini ya kitanda.

Taarifa ya uchunguzi wa kitaalam kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali imethibitisha kuwa paketi zote 163 zilikuwa na dawa za kulevya aina ya heroin ambazo jumla yake ni Kilogramu 174.77. Mtuhumiwa atafikishwa mahakamani mara baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Kwa upande wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya, Mamlaka inaendelea kufanya kaguzi za kufuatilia watu wanaokiuka taratibu za uingizaji na usambazaji wa kemikali bashirifu na dawa hizo ili kuzuia uchepushwaji. ambapo katika kipindi hicho kupitia mfumo wa kielektroniki (PEN-ONLINE SYSTEM) Mamlaka ilifanikiwa kuzuia uingizaji wa kilogramu 122,047.085 na Lita 85 za kemikali bashirifu.

Aidha, Mamlaka imeteketeza jumla ya hekari 21 za mashamba ya bangi mkoani Arusha na jumla ya kilogramu 250.7 za dawa za kulevya aina ya heroin na cocaine ambazo mashauri yake yalimalizika mahakamani, katika kiwanda cha saruji cha Dangote mkoani Mtwara.

Katika kuhakikisha jamii inapata elimu sahihi juu ya tatizo la dawa za kulevya; Mamlaka imeandaa muongozo utakaotumika kutoa elimu, imeshiriki kuandaa ujumbe juu ya tatizo la dawa za kulevya katika Mbio za Mwenge wa Uhuru zinazoendelea na kutoa elimu

kwa Kamati za Ulinzi na Usalama, kamati za Afya na watendaji wa Serikali za Mitaa ili wasaidie kuongeza uelewa wa tatizo la dawa za kulevya kwa jamii.

Tarehe 26 Juni kila mwaka, Tanzania huungana na Mataifa mengine kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya Duniani. Lengo likiwa ni kuongeza uelewa wa jamii na kuhamasisha Umma kushiriki katika mapambano dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya.


Mwaka huu Kitaifa maadhimisho haya yatafanyika jijini Dar es Salaam, katika viwanja vya Mnazi Mmoja na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb).

Kauli mbiu ya maadhimisho haya ni **“Tukabiliane na changamoto za dawa za kulevya kwa ustawi wa jamii”**

Maadhimisho haya kwa mwaka huu yatafanyika kuanzia tarehe 30 Juni kwa utoaji elimu na maonesho ya shughuli mbalimbali za udhibiti zinazofanywa na wadau mbalimbali katika udhibiti wa dawa za kulevya ambapo kilele cha Maadhimisho haya kitakuwa siku ya Jumamosi tarehe 02 Julai. Hivyo tunawaomba wananchi kushiriki katika Maadhimisho haya ili kupata elimu.

Mamlaka inawakumbusha wananchi kuwa, kujihusisha kwa namna yoyote ile na dawa za kulevya ni kosa kisheria. Sheria ya Kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya {Sura ya 95} inatoa adhabu kali hadi kifungo cha maisha kwa atayethibitika kujihusisha na kosa hilo. Hivyo basi, nitumie nafasi hii kuwataka wananchi kushiriki kwa dhati katika kukabiliana na tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya kwa kuwafichua wale wote wanaofanya biashara hiyo.

**Imetolewa na,**

  
Florence Khambi  
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

